# STANDARD SEVEN YEAR 2016

# END-TERM 2,

**KISWAHILI PAPER**
**1HR-40MINS**

Coordinated by KENPRO,
Macjo Arcade, 4th Floor, Suite 15E,
Off Magadi Road, Ongata Rongai |Tel: +254202319748 |
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website:www.schoolsnetkenya.com

# KISWAHILI TIME: 1HR-40MINS

**Chagua jibu sahihi kati ya yale uliyopewa kujaza nafasi zilizoachwa wazi.**

Wakati wa ______1______ jua lilitua na giza totoro ______2______. Kwa hivyo, nilipomaliza kukila ______3______. nilienda moja kwa moja hadi ______4______ chumba changu cha kulala. Mimi huyo! Nikajibwaga kitandani na kujifunika ______5______. Usingizi ______6______. Usingizi wa ______7______ ukanivamia na kunifanya ______8______.

1. A. machweo B. macheo C. mawio D. alfajiri
2. A. likatanda kote B. ukatanda wote C. ikatanda yote D. zikatanda zote
3. A. kistaftahi B. kishuka C. kinywaji D. kijio
4. A. penye B. kwa C. katika D. kwenye
5. A. fo! fo! fo! B. gubi gubi C. kocho kocho D. papatu papatu
6. A. nayo haikuchelewa B. nao haukuchelewa C. naye hakuchelewa D. nao haikuchelewa
7. A. mang'amung'amu B. lepe C. mang'amu D. pono
8. A. mfu B. maiti C. nusu-mfu D. mauti

Tangu serikali ianzishe elimu ______9______ katika shula za msingi za umma, kumekuwa na ______10______ katika idadi ya wanafunzi wanaojiunga na darasa la kwanza. Wengi hasa ______11______ watokao familia ______12______. Serikali imejitwika ______13______ kugharamia vifaa vyote vya shule ______14______ chaki, vitabu, madaftari na vingi vinginevyo. Kwa hivyo, sote tuungane ______15______ kuhakikisha kuwa kila mmoja anapata elimu

9. A. ya bure B. ya pesa C. ya ovyo D. ya maana
10. A. ongezeko B. upungufu C. ulegevu D. ufurufu
11. A. huyu huyu B. wale wale C. yule yule D. hawa hawa
12. A. tajiri B. erevu C. jinga D. hohe hahe
13. A. mamlaka ya B. jukumu la C. wadhifa wa D. uwezo wa
14. A. chambilecho B. waama C. mathalani D. aidha
15. A. bega kwa bega B. guu kwa guu C. ana kwa ana D. mkono kwa mkono



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

**Kutoka swali la 16 hadi 30 chagua jibu sahihi**

16. **Jaza pengo kwa usahihi.**

    Ingia _______________ ukaniletee kisu.

    A. kwa nyumbani
    B. katika nyumba
    C. kwa nyumba
    D. katika nyumbani

17. **Ni nini kinyume cha;**

    Makuli walipakia shehena usiku kucha.

    A. Makuli walipakua shehena usiku kucha
    B. Makuli walipakia shehena usiku kutwa
    C. Makuli walipakia shehena mchana kutwa
    D. Makuli walipakua shehena mchana kutwa

18. Ni vazi lipi kati ya yafuatayo lisilooana na mengine?

    A. Bulibuli    B. Kanchiri
    C. Gagro    D. Shati

19. Msanii ana mali _______________

    A. mengi    B. mingi
    C. nyingi    D. jingi

20. **Ni nini wingi wa;-**

    Mkunga alimvua mkunga.

    A. Mikunga waliwavua mikunga
    B. Mikunga walivua wakunga
    C. Wakunga waliwavua mikunga
    D. Wakunga walivua mikunga

21. Wazazi wa mume na mke huitana ________

    A. wacheja    B. wavyere
    C. wavyele    D. vivyere

22. Gurudumu lilibingirika mteremkoni ________

    A. hobela hobela
    B. kindaki ndaki
    C. bingiri bingiri
    D. pingiri pingiri

23. **Tumia "amba" katika sentensi ifuatayo;-**

    Kanisa lililojengwa ni kubwa.

    A. Kanisa ambalo lilijengwa ni kubwa
    B. Kanisa ambalo litajengwa ni kubwa
    C. Kanisa ambalo ilijengwa ni kubwa
    D. Kanisa ambayo ilijengwa ni kubwa

24. **Chagua sentensi iliyotumia kiunganishi kifaacho**

    A. Licha ya Ramadhan kuwa mwerevu, yeye ni mchoyo
    B. Usimdharau mtu fakaifani maskini
    C. Rangi ya ngozi yake si nyeusi wala nyekundu
    D. Ingawa Kamau ni mwerevu yeye ana adabu

25. Mzee Bakari amepigwa kalamu kazini. Maana yake ni ____________

    A. amepanda cheo kazini
    B. amefitiniwa kazini
    C. amestaafishwa kazini
    D. amefutwa kazi


26. Ni sentensi ipi inayooshewa wakati wa mazoea?

    A. Mwalimu wetu hufunza vizuri.
    B. Deno alikuwa akila chapati nilipofika kwake.
    C. Nitachezea taifa langu.
    D. Gari limeondoka kuelekea Kampala.

27. **Chagua sentensi inayoonyesha "ki' ya kielezi**

    A. Ukifika nyumbani msalimie mama.
    B. Kitito hiki ni kichafu sana.
    C. Utakapoenda Uhabeshi wataukwa wakivuna.
    D. Alipigana na jitu hilo kishujaa.

28. Kulingana na mchoro huu ni saa ngapi?



    A. saa mbili kasoro dakika ishiniri na tano
    B. saa nane kasoro dakika ishirini na tano
    C. saa nane kasoro dakika thelathini na tano
    D. saa mbili kasoro dakika thelathini na tano

29. Neno **"maktaba"** liko katika ngeli ya ________

    A. A - WA    B. YA - YA
    C. I - ZI    D. LI - YA

30. Mtu aliyezaliwa na upungufu wa akili huitwa ____

    A. mwendawazimu    B. mjinga
    C. bubu    D. punguani



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 - 40**

Ilikuwa alfajiri mapema tarehe kumi Julai mwaka jana nilipozinduliwa kutoka usingizini na mayowe yaliyotoka upande wa nyumba ya mama yangu. Moja kwa moja nikang'amua kuwa maskini mama alikuwa ashatuacha na kumrudia **mwenyezi Mungu**. Alikuwa akichungulia kaburi kwa wiki nzima na wakati huo wote alikuwa si hayati si mauti. Kwa hivyo, ilitubidi sisi wanawe kukaza roho mkononi. Maskini sisi!

Mimi huyo! Nikaenda shoti mpaka kwenye nyumba ya mama. "Wooooi! Wooooi! Mama....aa! Umeenda wapi mama! Mama uliyenipenda! mama uliyenipenda! Mama uliyenileta dunia hii ya madh............!" Niliangua kilio cha kwi! kwi! kwi! mithili ya mtu aliyepagawa na mashetani. Alimradi kamsa zilihinikiza kote bomani si majriani, si wajukuu, si vitukuu, si wanawe, si wakazawana, si marafikize, si wapwawe, kila mtu alichangia kumlilia mama. mama alikuwa mpenzi kwa wote. Alikuwa mwanamke aliyependwa kila mtu. Alikuwa mtu wa busara, mpole, mnyenyekevu, mwenye moyo mkunjufu na hususan hutambulisho chake kikubwa kilikuwa ni bidii zake zilizowaka moto. Zake zilizidi hata zile za mchwa wasemekano kwamba hujenga **vichuguu** kwa kutumia mate yao wenyewe.

Kweli, nisingemwona mama yangu tena! Akili zangu zilikataa kuamini kabisa. Mpaka leo, sijaamini kuwa sina mama. Akili bado zinanidanganya kwamba yeye aliendа matembezi tu na huenda akarudi. Hata hivyo, najaribu kwa udi na umbani kumsahau mama yangu kabisa. Kwani yaliyopita si ndwele, tugange yajayo. Kilocho muhimu ni kushughulikia maisha yetu ya usoni kwani huko ndiko tunakoelekea. Ya jana yamepita na kuenda kabisa. Chambilecho **wahenga**, maji yakimwangika hayazoleki.

31. Mayowe yaliyosikika asubuhi yalikuwa ya ______
    A. kuwaita watu kumsaidia mama ya mwandishi
    B. kuwaita watu kumpiga mwizi
    C. mama yake mwandishi kuchungulia kaburi
    D. mama yake mwandishi kwenda jongomeo
32. Neno Mwenyezi Mungu linaonyesha ______?
    A. mamlaka B. sifa
    C. heshima D. utajiri
33. Kuchungulia kaburi ni sawa na ______
    A. kunusurika kifo B. kutazama kaburini
    C. kuwa mahututi D. kuchimba kaburi
34. Ni bayana kwamba ______
    A. mwandishi alimkashifu mama yake
    B. mwandishi alimpenda mama yake
    C. mwandishi hakutarajia kifo cha mama yake
    D. mwandishi tu ndiye aliyempenda mama yake
35. Si kweli kusema kuwa ______
    A. mwandishi ndiye aliyekuwa mtoto wa kipekee wa mama huyo
    B. mama yake mwandishi alikuwa na wajukuu
    C. mama yake mwandishi alipendwa na watu wengi
    D. mama yake mwandishi alipendwa na majirani
36. Mama yake mwandishi hasa na tabia gani iliyotambulika kwa kila mtu?
    A. upole B. unyenyekevu
    C. busara D. bidii
37. Makao ya mchwa huitwa ______
    A. bumba B. bomba
    C. kichuguu D. kiota
38. Kutokana na taarifa ______
    A. mwandishi amemsahau mama yake kabisa
    B. mwandishi amejaribu kumsahau mama yake bila fanaka
    C. ni rahisi mwandishi kumsahau mama yake
    D. mwandishi hataki kumsahau mama yake
39. Kulingana na taarifa hii ______
    A. maisha ya siku za mbele ni muhimu sana
    B. maisha ya siku za mbele si muhimu sana
    C. tusisahau yaliyopita
    D. yaliyopita ni muhimu
40. Kichwa halisi cha habari hii ni ______?
    A. Siku ambayo sitaisahau
    B. Kifo cha mama
    C. Maji yakimwangika hayazoleki
    D. Yaliyopita si ndwele, tugange yajayo



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali 41 - 50**

Wasomi nawashukuru, kusoma kitabu hiki,
Mmakinike kihuru, mwelewe yanoghilibu,
Ya ulimwengu hudhuru, mwenzi sipojitanibu,
Dunia ni msumeno, hukata mbele na nyuma.

Ukipuuza kisomo, daima umo gizani,
Maisha yako kwa kimo, hali yako ni ya chini,
Kushangilia kisomo, sikipuuze moyoni,
Dunia ni msumeno, hukata mbele na nyuma.

Tuwaheshimu wazazi, walojitwika jukumu,
Wakijihini mavazi, waweze kutuhudumu,
Siku ukishika kazi, wakumbuke kihitimu,
Dunia ni msumeno, hukata mbele na nyuma.

Ujana ni jambo bora, ameupamba Rabana,
Kwako metia fora, utendalo hufanana,
Basi usiwe mkora, akiba uweke sana,
Dunia ni msumeno, hukata mbele na nyuma.

Maisha yana harufu, ile mbaya na nzuri,
Leo yakikusadifu, vyema kwako yanawiri,
Lakini yakikuhalifu, yataka upige dori,
Dunia ni msumeno, hukata mbele na nyuma.

Ni mimi bwana naimba, nakuusia yakini,
Himaya yangu ya heba, ni ya wangu eleweni,
Nawatakia ya huba, nilowaambia shikeni,
Dunia ni msumeno, hukata mbele na nyuma.

41. Shairi ulilolisoma ni la aina gani?
A. Tasdisa B. Takhmisa
C. Tarbia D. Tathlitha

42. Dhamira ya shairi hili ni ____________?
A. kuwakashifu vijana
B. kuwapongeza vijana
C. kuwasifu wazazi
D. kuwashauri vijana

43. Vina vya kati na vya mwisho vya ubeti wa nne ni __?
A. ra, na B. zi, mu
C. na, na D. fu, ri

44. Mshororo wa mwisho wa shairi hili huitwa _____?
A. kimalizio
B. ukwapi
C. utao
D. kibwagizo

45. Mwandishi anamaanisha nini anaposema ya kwamba maisha yana harufu mbaya na nzuri katika ubeti wa tano?
A. maisha hunuka na kununikia
B. maisha hayana harufu yoyote
C. maisha wakati mwingine huenda vizuri na pia yakaenda mrama
D. maisha ni kama chakula

46. Neno huba limetumika katika ubeti wa sita. Maana yake ni __________?
A. mapenzi B. chuki
C. hasira D. upole

47. Mshororo wa kwanza wa ubeti wa kwanza una mizani mingapi?
A. kumi na tano
B. kumi na minane
C. kumi na saba
D. kumi na sita

48. Stadi wa kutunga mashairi huitwa __________
A. Mkariri B. Mtunzi
C. Malenga D. Manju

49. Ni ubeti upi unaosisitiza umuhimu wa elimu?
A. wa kwanza B. wa pili
C. wa tatu D. wa nne

50. Kipande cha pili cha mshororo wa pili katika ubeti wa mwisho, "niya wangu eleweni" kitaitwa ____?
A. uteo B. ukwapi
C. mazda D. utao



Compiled by Schools Net Kenya
Available online at www.schoolsnetkenya.com | E-mail: infosnkenya@gmail.com | Mobile: 07 11 88 22 27